JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS - TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

HALMASHAURI YA WILAYA YA RUFIJI

# MKAKATI WA KUPUNGUZA VIHATARISHI VYA MAAFA

unicef for every child

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS – TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

**HALMASHAURI YA WILAYA YA RUFIJI**

# MKAKATI WA KUPUNGUZA VIHATARISHI VYA MAAFA

**MEI 2022**

**UIDHINISHAJI WA MKAKATI**

Mkakati wa Kupunguza Vihatarishi vya Maafa wa Halmashauri ya Wilaya ya Rufiji umeidhinishwa na:

25/05/2022

**John L. Kayombo**

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Rufiji na Mwenyekiti ya Kamati ya Wataalam ya Usimamizi wa Maafa ya Halmashauri

**Tarehe**

25/05/2022

**Mhe. Meja. Edward F. Gowele**

Mkuu wa Wilaya ya Rufiji na Mwenyekiti wa Kamati Elekezi ya Wilaya ya Usimamizi wa Maafa

**Tarehe**

**YALIYOMO**

UIDHINISHAJI WA MKAKATI ........................................ ii

ORODHA YA MAJEDWALI ........................................ iv

ORODHA YA MICHORO ........................................ v

DIBAJI ........................................ vi

SHUKURANI ........................................ vii

1 SEHEMU YA KWANZA ........................................ 1

1.1 Utangulizi ........................................ 1
1.2 Eneo la utawala na Jiografia ya Halmashauri ya Wilaya ya Rufiji ........................................ 1
1.3 Shughuli za kiuchumi na kijamii katika Halmashauri ya Wilaya ya Rufiji ........................................ 2
1.4 Uwepo wa vihatarishi na Uwezekano wa Kuathirika ........................................ 2

2 SEHEMU YA PILI ........................................ 3

2.1 Maono ........................................ 3

2.2 Dhima ........................................ 3

2.3 Madhumuni ........................................ 3

2.4 Malengo ya mkakati ........................................ 3

2.5 Miongozo ya Kufuata ........................................ 3

3 SEHEMU YA TATU: UCHAMBUZI WA HALI HALISI KATIKA HALMASHAURI ... 4

3.1 Hali ya Majanga ........................................ 4
3.2 Uwezekano wa Kuathirika na Majanga ........................................ 4
3.3 Uwezekano wa Kutokea kwa Majanga ........................................ 4
3.4 Sababu za Kutokea kwa Majanga ........................................ 6

3.5 Kuwepo Katika Eneo Hatarishi ........ 7
3.6 Uwezo wa kujiandaa na kukabili maafa ........ 9
3.7 Uchambuzi wa Uwezo, Fursa, Udhaifu na Changamoto ........ 10
4 SEHEMU YA NNE: UTEKELEZAJI WA MKAKATI ........ 12
4.1 Uelewa wa vihatarishi vya maafa ........ 12
4.2 Mfumo wa Tahadhari ya Awali ........ 13
4.3 Kuzuia, kupunguza vihatarishi na kujiandaa na maafa ........ 14
4.4 Uwezo wa Kukabili Maafa na Kurejesha Hali ........ 14
4.5 Ushirikishwaji na Uwajibikaji wa Jamii ........ 15
5 SEHEMU YA TANO: ........ 24
5.1 Mfumo wa Ufuatiliaji na Tathmini ........ 24
5.2 Viashiria vya Utendaji na Matokeo Tarajiwa ........ 24
5.3 Mpango wa Ufuatiliaji ........ 28
5.4 Utoaji wa Taarifa ........ 34
5.4.1 Mpango wa Ndani wa Utoaji Taarifa ........ 34
5.4.2 Mpango wa Utoaji Taarifa Nje ya Halmashauri (Mkoa na Taifa) ........ 35
6 SEHEMU YA SITA ........ 36
6.1 Mfumo wa Usimamizi wa Maafa ........ 36
6.2 Sera ya Taifa ya Menejimenti ya Maafa 2004 ........ 36
6.3 Sheria ya Usimamizi wa Maafa Sura 242 ........ 36
6.4 Muundo wa Usimamizi wa Maafa Katika Halmashauri ........ 36

**ORODHA YA MAJEDWALI**

Jedwali 1: Uwezekano wa Kutokea kwa Janga na Madhara ........ 5
Jedwali 2: Misimu ya Kutokea kwa Majanga ........ 5
Jedwali 3: Mali zilizopo katika vihatarishi ........ 7
Jedwali 4: Uwezo wa jamii kujiandaa na kukabili majanga ........ 9
Jedwali 5: Bangokitita la Utekelezaji wa Mkakati ........ 17
Jedwali 6: Viashiria vya utendaji wa mfumo wa ufuatiliaji na tathmini ........ 24
Jedwali 7: Mpango wa Ufuatiliaji ........ 29
Jedwali 8: Mpango wa Ndani wa Utoaji Taarifa ........ 34
Jedwali 9: Mpango wa Utoaji Taarifa Nje ya Halmashauri ........ 35

## ORODHA YA MICHORO

Mchoro 1: Muundo wa Usimamizi wa Maafa Tanzania ............................................ 37

**DIBAJI**

Halmashauri ya Wilaya ya Rufiji ipo katika uwezekano wa kupatwa na majanga ambayo yana vihatarishi mbalimbali kwa shughuli za kiuchumi na kijamii. Halmashauri ya Wilaya ya Rufiji inatambua kwamba ukubwa wa maafa hutegemea hali ya uwepo wa janga, uwezekano wa janga kusababisha vihatarishi na uwezo wa jamii wa kukabiliana na vihatarishi vya maafa yanayoweza kutokea. Uzoefu unaonesha kuwa majanga ya aina na viwango tofauti yamekuwa yakitokea katika halmashauri ya Wilaya ya Rufiji ikiwa ni pamoja na mafuriko, ukame, ajali za (moto, majini na barabarani), visumbufu vya mazao na uwepo wa wanyama pori wanaohatarisha maisha na mali. Majanga haya huifanya jamii kuwa katika hali hatarishi kila mwaka na hivyo kuhitaji mwitikio mkubwa katika usimamizi wake.

Hivyo, katika juhudi za kuwa na utayari wa usimamizi wa majanga na kukabiliana na maafa kwa ufanisi, Halmashauri ya Wilaya ya Rufiji kupitia ufadhili wa Shirika la Kuhudumia Watoto la Umoja wa Mataifa (UNICEF) kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu - Idara ya Uratibu wa Maafa imetambua umuhimu wa kuandaa Mkakati wa kupunguza vihatarishi vya maafa. Hali hii imechangiwa kwa kiasi kikubwa na vihatarishi vya mafuriko ambayo yamekuwa yakileta changamoto nyingi katika kukabiliana na maafa na kurejesha hali. Mkakati huu umeandaliwa kwa utaratibu wa kushirikisha Kamati Elekezi na Kamati ya Wataalam ya Usimamizi wa Maafa, na wadau wa maafa wa Wilaya hiyo. Mkakati unatoa mwongozo wa namna ya kuratibu na kusimamia upunguzaji wa vihatarishi vya maafa katika halmashauri ya Wilaya ya Rufiji.

Mkakati umejumuisha majanga yanayotokea mara kwa mara na kuainisha hatua mahususi za kuchukuliwa na Kamati Elekezi na Kamati ya Wataalam ya Usimamizi wa Maafa kwa halmashauri ya Wilaya ya Rufiji na wadau mbalimbali, zikiwemo taasisi za kiserikali na asasi zisizo za kiserikali katika kupunguza vihatarishi vya maafa. Aidha, Mkakati huu unaelezea majukumu ya kutekelezwa na idara, taasisi na wadau mbalimbali zilizopo kwenye Halmashauri ili kupunguza madhara ya maafa.

## SHUKURANI

Maandalizi ya Mkakati wa kupunguza vihatarishi vya maafa wa Halmashauri ya Wilaya ya Rufiji ni hatua muhimu za kujenga jamii iliyostahimilivu kwa kutambua kuwa Wilaya ya Rufiji ipo katika uwezekano wa kupatwa na majanga mbalimbali.

Tunatoa shukurani za dhati kwa Ofisi ya Waziri Mkuu kwa kushirikiana na kupitia ufadhili wa Shirika la Kuhudumia Watoto la Umoja wa Mataifa (UNICEF) katika kuwezesha uandaaji wa Mkakati huu na jitihada zao za jumla katika kuongeza uwezo wa Halmashauri ya Wilaya ya Rufiji katika usimamizi wa vihatarishi vya maafa na huduma za kibinadamu.

Kazi ya maandalizi ya Mkakati huu, imehusisha michango ya mawazo na mapendekezo ya kiutendaji na kitaalam iliyozingatia sheria, miongozo, taratibu na uzoefu kutoka kwa wadau mbalimbali katika Halmashauri ya Wilaya ya Rufiji. Bila ushirikiano na michango yao, isingekuwa rahisi kufikia hatua hii ya mwisho katika kuandaa Mkakati huu.

Tunapenda kutambua mchango mkubwa kutoka kwa Wakuu wa Idara na Vitengo na Wataalam wa Halmashauri ya Wilaya ya Rufiji, Mkoa wa Pwani, taasisi za serikali, asasi za kiraia na vyombo vya habari katika uandaaji wa Mkakati huu. Kwa namna ya pekee tunawashukuru Wenyeviti wa Kamati Elekezi na Kamati ya Wataalam ya Usimamizi wa Maafa ya Wilaya ya Rufiji kwa ushiriki wao katika shughuli nzima ya uandaaji wa Mkakati huu.

Mwisho, tunapenda kuwashukuru wataalam wawezeshaji Charles Msangi, Wilfrida Ngowi, Ally Mwatima, Ewald Bonifasi na Makulu N. Butondo kutoka Ofisi ya Waziri Mkuu na Mtaalam Mwelekezi Vivaoliva Shoo kwa kutekeleza jukumu la kuongoza kazi ya kuandaa Mkakati huu bila kuchoka.

**John L. Kayombo**

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Rufiji na Mwenyekiti ya Kamati ya Wataalam ya Usimamizi wa Maafa ya Halmashauri

# SEHEMU YA KWANZA

## 1.1 Utangulizi

Halmashauri ya Wilaya ya Rufiji ipo katika uwezekano wa kupatwa na majanga ambayo yanaweza kusababisha vihatarishi mbalimbali kwa shughuli za kiuchumi na kijamii. Halmashauri hii inatambua kwamba ukubwa wa maafa hutegemea hali ya uwepo wa janga, uwezekano wa janga kusababisha vihatarishi na uwezo wa jamii wa kukabili vihatarishi vya maafa yanayoweza kutokea. Tathmini ya vihatarishi, uwezekano wa kutokea na uwezo wa kukabili maafa iliyofanyika katika Halmashauri ya Wilaya ya Rufiji inaonesha kuwa Wilaya ya Rufiji imekuwa ikipatwa na maafa yanayosababishwa na majanga ya mafuriko, ukame, ajali za (moto, majini na barabarani), magonjwa ya mlipuko, wanyamapori, wadudu na ndege waharibifu, na migogoro kati ya wakulima na wafugaji. Majanga haya, huifanya jamii kuwa katika hali hatarishi kila mwaka na hivyo kuhitaji mwitikio mkubwa katika usimamizi wake.

Majanga hayo huchagizwa zaidi na mabadiliko ya tabianchi ndani na nje ya Halmashauri, kuongezeka kwa idadi ya shughuli za kiuchumi kwenye maeneo yanayokabiliwa na majanga, uwepo wa makazi katika bonde la mto Rufiji na sehemu kubwa ya Halmashauri ya Wilaya ya Rufiji eneo lake ni tambarare. Maafa ya hivi karibuni yamesababishwa na mafuriko, magonjwa ya mlipuko, ukame pamoja na ajali za barabarani. Matokeo ya athari hizo zimesababisha upotevu wa maisha, mali, uharibifu wa miundombinu ya kijamii na kiuchumi na mazingira kwa ujumla.

## 1.2 Eneo la utawala na Jiografia ya Halmashauri ya Wilaya ya Rufiji

Halmashauri ya Wilaya ya Rufiji Kaskazini imepakana na Halmashauri za Wilaya ya Kisarawe na Kibiti, Mashariki imepakana na Kibiti, Kusini imepakana na Halmashauri ya Wilaya ya Kilwa (Mkoa wa Lindi), Kusini-Magharibi imepakana na Wilaya ya Liwale na Magharibi imepakana na Mkoa wa Morogoro. Halmashauri ya Wilaya ya Rufiji ina eneo lenye ukubwa wa kilomita za mraba 9,485. Takriban kilomita za mraba 1,656.62 ni hifadhi za misitu huku Pori la Akiba la Selous lina ukubwa wa kilomita za mraba 6,258. Ni takriban kilomita 200 kusini mwa Dar es salaam. Wilaya hii ina idadi ya tarafa 3, Kata 13, mamlaka ya mji 1, vijiji 38, vitongoji 177 na kaya 28,956.

Wilaya ya Rufiji imegawanywa na mto mkubwa wa Rufiji utokao Magharibi na kuelekea Mashariki kwenye bahari ya Hindi. Wilaya hii imegawanyika katika kanda kuu mbili ambazo ni Kanda ya bonde la mafuriko la mto Rufiji (Flood Plain), ni ukanda unaopata mafuriko mara kwa mara ukiwa na urefu wa Km. 130 kutoka Magharibi hadi Mashariki na upana wa wastani kati ya km. 7-35. Katika ukanda huu kuna mabwawa/maziwa (oxbow lakes) takribani 13.

Ukanda wa pili ni ukanda wa juu. Wilaya ya Rufiji inapata wastani wa milimita 800 – 1,200 za mvua kwa mwaka.

### 1.3 Shughuli za kiuchumi na kijamii katika Halmashauri ya Wilaya ya Rufiji

Uchumi wa Halmashauri ya Wilaya ya Rufiji unategemea shughuli za kilimo, uvuvi, ufugaji, biashara kubwa na ndogo ndogo, ajira rasmi na isiyo rasmi (vibarua) katika pori la Selous. Uchumi huu unawezesha jamii kukidhi mahitaji ya msingi katika familia na kujiletea maendeleo. Pori la hifadhi la Selous, Chemichemi ya maji moto ni vivutio vya utalii vinavyoongeza pato la Halmashauri. Mazao ya chakula na biashara yanayolimwa ni korosho, nazi, ufuta, mihogo, mahindi, maharage, mtama, mpunga, mbogamboga na mtama. Matunda yanayolimwa ni machungwa, mapapai na mananasi ni mengi.

### 1.4 Uwepo wa vihatarishi na Uwezekano wa Kuathirika

Uwezekano wa kuathirika unatokana na uwepo wa majanga ya mafuriko, uvamizi wa wanyama pori, ukame, ajali za (moto, majini na barabarani), wadudu waharibifu, migogoro kati ya wakulima na wafugaji. Aidha, uwepo wa watu, makazi na shughuli za kiuchumi katika maeneo ya karibu na bonde la Mto Rufiji, uwepo wa miundombinu duni na mbuga ya wanyama ya Selous inaiweka jamii katika uwezekano mkubwa wa kuathirika.

# SEHEMU YA PILI

## 2.1 Maono

Kuwa na uchumi imara na endelevu, utakaowezesha kukuza maendeleo ya jamii kuwa na maisha bora, huduma bora na endelevu za kijamii, miundombinu yenye usalama, umoja na amani.

## 2.2 Dhima

Kuimarisha maendeleo ya uchumi wa jamii kwa utoaji wa huduma bora na endelevu, miundombinu, usalama, umoja na amani

## 2.3 Madhumuni

Madhumuni ya mkakati huu ni kuweka hatua za kuzuia na kupunguza vihatarishi vya majanga ili kujenga jamii stahimilivu kwa maafa. Mkakati huu unazingatia utekelezaji wa mzingo wa usimamizi maafa na ushiriki wa kila sekta katika kupunguza vihatarishi vya majanga ili kufanikisha maendeleo endelevu katika Wilaya ya Rufiji.

## 2.4 Malengo ya mkakati

(a) Kuongeza uelewa wa upunguzaji wa vihatarishi vya maafa kwa jamii, sekta na wadau katika ngazi ya wilaya;

(b) Kuboresha mfumo wa tahadhari ya awali ili kujiandaa na majanga mbalimbali na utoaji wa taarifa zenye kujikita katika jamii;

(c) Kuimarisha uwezo wa kuzuia, kupunguza vihatarishi na kujiandaa kukabiliana na maafa ili kujenga ustahimilivu katika jamii;

(d) Kuimarisha uwezo wa kukabili na kurejesha hali baada ya maafa kutokea; na

(e) Kujenga ustahimilivu kwa jamii kupitia ushirikishaji na uwajibikaji wa wanajamii katika kuzuia, kupunguza, kujiandaa na kukabili maafa.

## 2.5 Miongozo ya Kufuata

(i) Kuzingatia mila, desturi na tamaduni zilizopo katika masuala ya usimamizi wa maafa;
(ii) Utekelezaji wa Mkakati huu utaenda sambamba na utekelezaji wa majukumu ya kawaida ya Idara/Sekta zilizopo kwenye Halmashauri; na
(iii) Malengo na shabaha za mkakati huu yatajumuishwa kwenye mipango ya maendeleo na mpango wa bajeti wa Halmashauri.

# SEHEMU YA TATU: UCHAMBUZI WA HALI HALISI KATIKA HALMASHAURI

## 3.1 Hali ya Majanga

Tathmini ya vihatarishi, uwezekano wa kutokea na uwezo wa kukabili maafa iliyofanyika katika Halmashauri ya Wilaya ya Rufiji inaonesha kuwa Wilaya ya Rufiji imekuwa ikipatwa na maafa yanayosababishwa na majanga ya mafuriko, ukame, ajali za (moto, majini na barabarani), magonjwa ya mlipuko, wanyama pori, wadudu na ndege waharibifu, na migogoro kati ya wakulima na wafugaji.

## 3.2 Uwezekano wa Kuathirika na Majanga

Uwezekano wa kuathirika unatokana na uwepo wa majanga ya mafuriko, uvamizi wa wanyama pori, ukame, ajali za (moto, majini na barabarani), wadudu waharibifu, migogoro kati ya wakulima na wafugaji.

Uwezekano wa kuathirika na mafuriko inachangiwa na Halmashauri hii kuwa katika ukanda unaozungukwa na bonde la Mto Rufiji ambao hupokea maji kutoka mito ya Kilombero na Ruaha na mito mingine midogo midogo. Ongezeko la kuathiriwa linachangiwa zaidi na uwepo wa watu, makazi na shughuli za kiuchumi katika maeneo ya karibu na bonde la Mto huo.

Vilevile, uwepo wa Wanyama wakali na wadudu na ndege waharibifu katika Pori la Akiba la Selous wamekuwa tishio kwa maisha ya watu na usalama wa chakula. Wilaya ya Rufiji pia imekuwa ikikabiliwa na upungufu wa mvua hivyo kuongeza uwezekano wa kutokea kwa ukame. Hali hii inachangiwa na mabadiliko ya tabianchi.

## 3.3 Uwezekano wa Kutokea kwa Majanga

Wilaya ya Rufiji imekuwa ikipatwa na majanga ya mafuriko, ukame, ajali za (moto, majini na barabarani), Wanyama na ndege waharibifu na migogoro ya wakulima na wafugaji. Jedwali lifuatalo linaonesha uwezekano wa kutokea kwa janga na makadirio ya athari kwa jamii na mali na misimu ambayo majanga hayo hutokea.

**Jedwali 1: Uwezekano wa Kutokea kwa Janga na Madhara**

| NA. | AINA YA JANGA | | UWEZEKENO WA KUTOKEA JANGA | | | MADHARA YA MAJANGA KWA JAMII | | | ATHARI ZA JANGA KWA MALI | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | juu | kati | chini | Juu | kati | chini | juu | kati | chini |
| 1. | Mafuriko | | √ | | | √ | | | √ | | |
| 2. | Ukame | | | √ | | | | √ | | | √ |
| 3. | Wanyama | Wakali/pori | √ | | | | √ | | √ | | |
| | | Waharibifu | | √ | | √ | | | | | √ |
| 4. | Wadudu waharibifu | | | | √ | | | √ | | | √ |
| 5. | Milipuko ya magonjwa | | | | √ | | | √ | | | √ |
| 6. | Ndege waharibifu | | | | √ | | | √ | | | √ |
| 7. | Migogoro ya wakulima na wafugaji | | √ | | | √ | | | | √ | |
| 8. | Ajali za | Moto | √ | | | √ | | | √ | | |
| | | Barabarani | | | √ | | √ | | | √ | |
| | | Majini | | √ | | | √ | | | √ | |
| 9. | Panya | | | | √ | | | √ | | | √ |

**Chanzo:** Kikao cha Wataalam wa Halmashauri ya Wilaya ya Rufiji na Tathmini katika ngazi ya vijiji (Nyamakurukuru, Ngarambe, Mohoro na Chumbi A), Aprili, 2022

**Jedwali 2: Misimu ya Kutokea kwa Majanga**

| Na | Aina ya Janga | | Kipindi cha kutokea majanga | | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | Jan | Feb | Ma | Apr | Mei | Juni | Jul | Aug | Sept | Okt | Nov | Des |
| 1. | Mafuriko | | | | | | | | | | | | | |
| 2. | Ukame | | | | | | | | | | | | | |
| 3. | Wanyamapori | Wakali/pori | | | | | | | | | | | | |
| | | waharibifu | | | | | | | | | | | | |
| 4. | Wadudu waharibifu | | | | | | | | | | | | | |
| 5. | Milipuko ya magonjwa | | | | | | | | | | | | | |
| 6. | Ndege waharibifu | | | | | | | | | | | | | |
| 7. | Migogoro ya wakulima na wafugaji | | | | | | | | | | | | | |
| 8. | Ajali za | Barabarani | | | | | | | | | | | | |
| | | majini | | | | | | | | | | | | |
| | | moto | | | | | | | | | | | | |
| 9. | Panya | | | | | | | | | | | | | |

**Chanzo:** Kikao cha Wataalam wa Halmashauri ya Wilaya ya Rufiji na Tathmini katika ngazi ya vijiji (Nyamakurukuru, Ngarambe, Mohoro na Chumbi A), Aprili, 2022.

## 3.4 Sababu za Kutokea kwa Majanga

### (i) Sababu za kijiografia

Halmashauri ya Wilaya ya Rufiji ina jumla ya eneo la kilomita za mraba 9,485 linalojumuisha nchi kavu na maji. Wilaya hii imegawanyika katika kanda kuu mbili ambazo ni uwanda wa mafuriko wa mto Rufiji (Flood Plain) na uwanda wa juu. Uwanda wa mafuriko ni ukanda unaopata mafuriko mara kwa mara ukiwa na urefu wa kilomita 130 kutoka Magharibi hadi Mashariki na upana wa wastani kati ya kilometa 7-35. Mafuriko husabibishwa na kujaaa au kupasuka kwa kingo za mto Rufiji ambao unapokea maji kutoka maeneo mbalimbali ya nchi ikiwemo Mto Ruaha Mkuu, Mto Kilombero na mito mingine inayomwaga maji kwenye mto huo. Mto Ruaha Mkuu na Mto Kilombero hupeleka maji yake kwenye mabwawa ya kufua umeme ya Mtera na Kidatu ambapo inapotokea kujaa kwa mabwawa haya hulazimika kufunguliwa milango yake na kusababisha maji hayo kufurika katika mto Rufiji na kusambaa kwenye mashamba na Makazi ya Watu.

Vilevile, Wilaya inalo eneo kubwa la Hifadhi za misitu na imepakana na pori la akiba la Selous kwa upande wa magharibi. Kata zilizopakana na Pori la Akiba la Selous ni Ngarambe, Mwaseni, Chemchem na Utete. Uwepo wa pori hili kwa kiasi kikubwa umeongeza mwingiliano wa shughuli za kibinadamu, wanyama na ndege waharibifu ambao kwa kiasi kikubwa unaongeza tishio kwenye maisha ya watu na usalama wa chakula. Hali huwa mbaya zaidi kipindi ambacho kuna ukame na wakati wa mavuno kutokana na ongezeko la uvamizi wa wanyama pori ambao wanatafuta chakula na maji.

### (ii) Hali ya kiuchumi

Uchumi wa Halmashauri ya Wilaya ya Rufiji unategemea zaidi shughuli zinazofanyika katika bonde la mto Rufiji na Pori la Akiba la Selous. Shughuli hizo ni pamoja na kilimo, uvuvi, ufugaji, biashara na ajira rasmi na zisizo rasmi katika pori la Selous. Shughuli za kilimo zimekuwa zikichangia katika kuongeza uwezekano wa kutokea kwa majanga kutokana wananchi kulima karibu na kingo za mito hali inayosababisha kupungua kwa uimara wa kingo, kupungua kwa kina cha mto na hivyo kubomoka pindi maji yanapojaa na kusababisha mafuriko kwenye maeneo ya mashamba na makazi.

Uwepo wa eneo la pori linaloweza kutumika kwa malisho ya mifugo kumechangia ongezeko la wafugaji katika Wilaya hiyo. Hali imekuwa ikichangia migogoro ya wakulima na wafugaji hususani kipindi cha

kiangazi ambacho makundi yote mawili yanategemea vyanzo vilevile vya maji ambavyo pia vipo karibu na mashamba ya wakulima. Vilevile jamii imekuwa ikijishughulisha na uchomaji wa mkaa unaosababisha uvunaji holela wa miti hali ambayo inachangia uharibifu wa mazingira unaoweza kuleta ukame katika maeneo hayo.

**(iii)Uelewa Mdogo Kuhusu Masuala ya Maafa**

Tathmini ya Vihatarishi, Uwezekano wa Kuathirika na Uwezo wa kukabili maafa ilionesha kuwa jamii haina uelewa wa kutosha kuhusu hatua za kuchukua katika kuzuia, kupunguza madhara, kujiandaa na kukabiliana na maafa. Hali hii imesababisha wananchi kuweka makazi ya kudumu na kufanya shughuli za kiuchumi katika maeneo hatarishi bila kuzingatia vihatarishi vilivyopo na kuchukua hatua za kujikinga.

## 3.5 Kuwepo Katika Eneo Hatarishi

Zipo rasilimali, makazi na miundombinu ya huduma mbalimbali za jamii katika maeneo hatarishi hali inayofanya rasilimali hizo kuwa katika hatari ya kukubwa na maafa. Jedwali lifuatalo linaonesha jamii na rasilimali zilizopo kwenye maeneo hatarishi.

**Jedwali 3: Mali zilizopo katika vihatarishi**

| | Mali /Watu | Janga | Eneo Hatarishi na Takwimu |
|---|---|---|---|
| 1 | Watu na Makazi | Mafuriko | Takribani watu 108,625 sawa na asilimia 93.8 ambazo ni sawa na jumla ya kaya 27,156 wanaishi katika maeneo hatarishi katika kata za Utete, Ngarambe, Chumbi, Mgomba, Umwe, Ikwiriri, Ngorongo, Mkongo Mohoro, Mwaseni, Mbwara na Kipugira |
| | | Wanyama Wakali | Takribani watu 43,662 sawa na asilimia 37.7 ambazo ni sawa na jumla na kaya 10,916 wanaishi katika maeneo hatarishi katika kata za Ngarambe, Utete, Mwaseni, Chemchem Ngorongo, Mkongo na Kipugira. |
| | | Migogoro ya Wakulima na Wafugaji | Takribani watu 115,825 sawa na asilimia 100 ambazo ni sawa na jumla na kaya 28,956 wanakabiliwa na migogoro katika kata za Utete, |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | | Chemchem, Mbwara, Mwaseni, Chumbi, Kipugira, Mgomba, Ngorongo, Mkongo, Umwe, Ikwiriri, Ngarambe na Mohoro. |
| | | Moto | Kata 13 za Halmashauri zipo hatarini kukumbwa na ajali za moto iwapo utatokea |
| 2 | Mashamba | Mafuriko | Jumla ya hekta 36,039.85 za mashamba ya mazao aina mbalimbali katika kata za Utete, Ngarambe, Chumbi, Mgomba, Umwe, Ikwiriri, Ngorongo, Mkongo, Kipugira, Mwaseni, Mbwara na Mohoro |
| | | Ukame | Jumla ya ekari za mashamba zipatazo 15,650 katika kata za Mwaseni, Kipugira, Ngorongo, Ngarambe, Mbwara na Mkongo zipo katika maeneo hatarishi kwa ukame |
| | | Wanyama na Ndege waharibifu | Jumla ya ekari za mashamba zipatazo 12,539.9 katika kata za Ngarambe, Utete, Mwaseni, Chemchem, Ngorongo na Kipugira zipo katika maeneo hatarishi kwa Wanyama na ndege waharibifu. |
| 3 | Majengo ya Zahanati | Mafuriko | Kituo cha afya cha Mohoro kilichopo kata ya Mohoro kipo katika eneo lenye historia ya kupata mafuriko. |
| 4 | Majengo ya Shule | Mafuriko | Shule ya Umwe Sekondari hushindwa kufikika wakati wa mafuriko kutokana na barabara kukatika;<br>Shule za Msingi za Nyampaku, Mohoro, Ngarambe, Ndundutawa, Kipoka na King’ongo zilizopo katika Kata ya Mohoro zina historia ya kuzingirwa na maji ya Mafuriko |
| 5 | Madaraja na Barabara | Mafuriko | Vipande vya barabara vyenye wastani wa kilometa 10 vinaathirika na mafuriko kutoka barabara za<br>Nyamwage – Utete; na Mkongo - Mloka;<br>Daraja la Mohoro, Ngaro, |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | | Mtanzamsona, mchangini na Mbambe huwa yanafurika Maji; |
| 6 | Minara ya Simu | Mafuriko | Aina ya Minara 5 ya simu ipo katika kata ya mhoro, kwenye maeneo ya mafuriko. |

### 3.6 Uwezo wa kujiandaa na kukabili maafa

Jedwali lifuatalo linaainisha majanga, uwezo wa jamii katika kujiandaa na kukabili majanga hayo na changamoto zilizopo.

**Jedwali 4: Uwezo wa jamii kujiandaa na kukabili majanga**

| | Janga | Uwezo wa jamii | Changamoto |
|---|---|---|---|
| **1** | **Mafuriko** | (i). Kusaidiana wao kwa wao katika kupeana hifadhi kutokana na maafa;<br>(ii). Pindi mazao yao yanaposombwa na maji, wananchi hutumia chakula mbadala ikiwemo ndizi na kufanya biashara ndogondogo kama vile kuuza korosho;<br>(iii). Tahadhari ya awali kwa njia ya kiasili ambapo ndege wa aina fulani huhama kwenye bonde la Mto Rufiji hali inayoashiria mafuriko;<br>(iv). Kupeana taarifa kutoka vijiji ambavyo maji ya mafuriko hutangulia kufika | (i). Jamii haina uwezo wa utafutaji na uokoaji hivyo kuhitaji msaada wa taasisi zanye uwezo huo;<br>(ii). Jamii haina uelewa wa hatua za kuchukua kujiandaa na kukabili maafa; na<br>(iii). Jamii haina timu za kukabiliana na dharura; |
| **2** | **Ukame** | (i). Uwepo wa mto Rufiji unaweza kusaidia katika kilimo cha umwagiliaji;<br>(ii). Ecolojia ya Kilimo ya | (i). Utamaduni jamii kulima aina Fulani ya mazao hivyo kutokubali ushari wa wataalam kulima mazao yanayostahimili ukame. |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | wilaya ya Rufiji inaruhusu kilimo cha mazao yanayostamili ukame kama vile mihogo<br>(iii). Uwepo shughuli za uvuvi ambazo zinaweza kuchangia upatikanaji wa chakula mbadala kwa kuuza Samaki ili kujipatia kipato<br>(iv). Ujuzi wa mbinu ya asili ya kutabiri uwepo wa ukame katika msimu unaofuata ambapo uwepo wa wadudu wanaoshambulia mazao huwa ni tahadhari ya awali ya ukame; | (ii). Utayari wa jamii kupunguza mifugo kipindi cha ukame<br>(iii). Jamii haina uelewa wa hatua za kuchukua kujiandaa na kukabili maafa |
| 3 | **Wanyama pori** | Jamii inatumia mbinu za kienyeji kukabiliana na wanyama pori | Kata za Ngarambe, Utete, Mwaseni, Chemchem Ngorongo na Kipugira zimepakana na Hifadhi ya Selous; |
| 4 | **Magonjwa ya mlipuko** | Uwepo wa zahanati na vituo vya afya karibu na maeneo ya wananchi.<br>Uwepo wa elimu ya kujikinga na magonjwa ambukizi mfano: kunawa mikono mara kwa mara n.k. | Uelewa mdogo kuhusu hatua za kuchukua kuzuia, kupunguza, kujiandaa na kukabiliana na magonjwa ya mlipuko |

## 3.7 Uchambuzi wa Uwezo, Fursa, Udhaifu na Changamoto

Uchambuzi umefanywa kwa kutambua uwezo uliopo, fursa zilizopo, udhaifu na changamoto kama msingi wa uundaji wa malengo ya mkakati huu. Uchambuzi utasaidia kuchukua hatua zinazofaa na madhubuti za upunguzaji

wa vihatarishi vya maafa ili kuokoa maisha ya watu, mali na kulinda mazingira kwa sasa na siku zijazo. Uchambuzi huo ni kama inavyoonekana kwenye jedwali Na.2 hapo chini

| **Uwezo** | | **Fursa** |
|---|---|---|
| Uwepo wa Mratibu wa Maafa wa Wilaya | | Uwepo ujenzi wa mradi mkubwa wa kuvua umeme wa Stiegler's George |
| Uwepo wa Boti za Uokoaji | | Uwepo wa vivutio vya kitalii – chemchem ya maji moto, pori la akiba la selous |
| Uwepo wa Mpango wa Matumizi Bora ya Ardhi | | Uwepo wataalam wa Usimamizi wa Maafa ngazi ya Taifa na MKoa |
| Uwepo mfumo wa kisheria wa Usimamizi wa Maafa kutoka ngazi ya Wilaya hadi Kijiji | | Uwepo wa mahusiano mazuri baina ya Halmashauri, taasisi zilizopo, wadau na jamii kwa ujumla |
| Uwepo wa miundombinu ya barabara na mawasiliano | | Uwepo wa wataalam wa kikanda wa mamlaka ya hali ya hewa |
| Uwepo wa Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Wilaya | | Uwepo wa taasisi za kifedha |
| | | Uwepo wa wataalam wa hifadhi ya wanyama pori Selous |
| | | Uwepo wa Sera, Sheria na miongozo ya Usimamizi wa Maafa. |
| | | Uwepo wa Mamlaka ya Uendelezaji wa Bonde la Mto Rufiji |
| | | Uwepo wa Mamlaka ya Usimamizi wa Bonde la Ruvuma na Pwani ya Kusini |
| **Udhaifu** | | **Changamoto** |
| Uelewa mdogo wa masuala ya usimamizi wa maafa kwa jamii na Kamati za Usimamizi wa Maafa | | Kutokea kwa maafa ya mafuriko kila mwaka |
| Kubadilika kwa waratibu wa Maafa wa Halmashauri kutokana na mabadiliko ya majukumu na vituo vya kazi | | Eneo la Uratibu wa maafa kutotengewa bajeti |
| Kutofuatwa kwa miongozo, sera, sheria za Usimamizi wa maafa | | Uwepo wa migogoro ya wakulima na wafugaji |
| Ujenzi wa miundombinu ya jamii na makazi kwenye maeneo hatarishi | | Miundombinu hafifu ya barabara, madaraja yanayounganisha Kijiji na Kijiji |
| Uendeshaji wa shughuli za kiuchumi kwenye maeneo hatarishi | | |
| Ukosefu wa timu ya dharura ya | | |

| | | |
|---|---|---|
| wataalam ya kukabiliana na dharura za maafa | | |

**SEHEMU YA NNE: UTEKELEZAJI WA MKAKATI**

## 4.1 Uelewa wa vihatarishi vya maafa

### (a) Lengo

Kuongeza uelewa wa upunguzaji wa vihatarishi vya maafa kwa jamii, sekta na wadau katika ngazi ya wilaya

### Mikakati

(i). Kujenga uelewa kuhusu masuala ya upunguzaji wa vihatarishi vya maafa kwa kamati za usimamizi wa maafa, wadau na jamii;
(ii). Kufanya tathmini za kabla, wakati na baada ya maafa kutokea katika Wilaya;
(iii). Kufanya tafiti za Vihatarishi vya Maafa kwa kushirikiana na wadau mbalimbali wa usimamizi wa maafa waliopo katika Wilaya;
(iv). Wilaya kukuza matumizi ya TEHAMA na huduma za kijiografia katika usimamizi wa vihatarishi vya maafa.

**Shabaha**

(i). Elimu kwa Kamati za Usimamizi wa Maafa ngazi ya Wilaya hadi Kijiji kutolewa ifikapo 2027;
(ii). Uhamasishaji wa kukuza uelewa wa vihatarishi vya maafa kwenye maeneo hatarishi kufanyika ifikapo Juni, 2027;
(iii). Maeneo hatarishi kubainishwa ifikapo, Juni 2027;
(iv). Uwezo wa Halmashauri kukabili na kubaini Maafa ifikapo Juni, 2027;
(v). Tathmini za uharibifu na mahitaji wakati wa maafa kufanyika ifikapo Juni, 2027;
(vi). Uharibifu na hasara kutokana na maafa kutambuliwa ifikapo juni, 2027;
(vii). Tafiti za visababishi vya maafa yanayojirudia kufanyika ifikapo Juni, 2027;
(viii). Mifumo ya TEHAMA kutumika katika usimamizi wa maafa ifikapo Juni, 2027;
(ix). Ramani za maeneo hatarishi na maeneo ya uhamishaji kuandaliwa ifikapo Juni, 2027;

## 4.2 Mfumo wa Tahadhari ya Awali

**(b) Lengo**

Kuboresha mfumo wa tahadhari ya awali ili kujiandaa na majanga mbalimbali na utoaji wa taarifa zenye kujikita katika jamii.

**Mkakati**

(i). Kutumia maarifa ya asili kwenye mfumo wa utoaji wa tahadhari ya awali;
(ii). Kuwepo na mfumo rasmi wa utoaji na upokeaji wa taarifa za tahadhari ya awali kuanzia ngazi ya Halmashauri, kata na kijiji, na jamii kwa ujumla;

**Shabaha**

(i). Maarifa na mbinu za kiasili zinazotumika kupata tahadhari ya awali kubainishwa ifikapo Juni, 2027;
(ii). Maarifa na mbinu za asili kuboreshwa na kujumuishwa kwenye mfumo rasmi wa utoaji wa tahadhari ifikapo Juni 2027;
(iii). Taratibu za uendeshaji na itifaki kwa ajili ya utoaji na usambazaji wa tahadhari za awali kuandaliwa ifikapo Juni, 2027;

## 4.3 Kuzuia, kupunguza vihatarishi na kujiandaa na maafa

**(c) Lengo**

Kuimarisha uwezo wa kuzuia, kupunguza vihatarishi na kujiandaa kukabiliana na maafa ili kujenga ustahimilivu katika jamii.

**Mikakati**

(i). Kuandaa na kutekeleza programu za upunguzaji wa vihatarishi vya majanga yanayoikumba Halmashauri;
(ii). Kutambua rasilimali zinazoweza kutumika kukabiliana na maafa katika Halmashauri;
(iii). Kufanya mazoezi ya vitendo kwa ajili ya kujiandaa na kukabili maafa;
(iv). Kuimarisha huduma za utafutaji na uokoaji katika Halmashauri kwa kuzingatia majanga yaliyopo;

**Shabaha**

(i). Mpango wa matumizi bora ya ardhi kutekelezwa ifikapo Juni, 2027

(ii). Programu za mafunzo ya kupunguza vihatarishi ya majanga kutekelezwa ifikapo Juni, 2027;

(iii). Watu wanaoishi katika maeneo hatarishi kutambuliwa na kuhamishwa ifikapo Juni, 2027;

(iv). Kanzidata ya wadau na rasilimali za kukabiliana na maafa kuandaliwa ifikapo Juni, 2027;

(v). Timu za utafutaji na uokoaji kuanzishwa ifikapo Juni, 2027;

(vi). Upatikanaji wa vifaa vya utafutaji na uokoaji ifikapo Juni 2027;

(vii). Mazoezi ya mezani na vitendo ya kujiandaa na kukabili maafa kufanyika ifikapo Juni, 2027;

(viii). Njia za kupita wakati wa uhamishaji kuainishwa ifikapo Juni, 2027;

(ix). Maeneo salama kwa ajili ya kuhamishia watu wakati wa dharura kutambuliwa na kutengwa ifikapo Juni, 2027;

(x). Maeneo yanayofaa kwa ajili ya huduma ya matibabu ya dharura kwa magonjwa ya mlipuko kutambuliwa na kutengwa ifikapo Juni, 2027;

## 4.4 Uwezo wa Kukabili Maafa na Kurejesha Hali

**(d) Lengo**

Kuimarisha uwezo wa kukabili na kurejesha hali baada ya maafa kutokea.

**Mikakati**

(i). Kufanya tathmini za uharibifu na mahitaji baada ya maafa kutokea;

(ii). Kuhamasisha upatikanaji wa rasilimali kwa ajili ya kukabiliana na kurejesha hali baada ya maafa;

(iii). Kutekeleza muongozo wa utoaji wa huduma za kibinadamu wakati wa maafa;

**Shabaha**

(i). Tathmini ya haraka ya uharibifu na mahitaji wakati wa maafa kufanyika ifikapo Juni, 2027;

(ii). Tathmini ya kina ya uharibifu na mahitaji baada ya maafa kufanyika ifikapo Juni, 2027;

(iii). Wadau kuhamasishwa kushiriki na kutoa rasilimali kwa ajili ya operesheni za kukabiliana na maafa ifikapo Juni, 2027;

(iv). Huduma za kibinadamu kwa waathirika wa maafa kutolewa kwa kuzingatia muongozo ifikapo Juni, 2027;

(v). Huduma za usaidizi wa kisaikolojia na kurekebisha afya ya akili kwa waathirika wa maafa na watoa huduma ifikapo Juni, 2027;

## 4.5 Ushirikishwaji na Uwajibikaji wa Jamii

**(e) Lengo**

Kujenga ustahimilivu kwa jamii kupitia ushirikishaji na uwajibikaji wa wanajamii katika kuzuia, kupunguza, kujiandaa na kukabili maafa;

**Mikakati**

(i) Kutumia ujuzi wa jamii katika kuzuia, kupunguza, kujiandaa, kukabili maafa na kurejesha hali baada ya maafa;

(ii) Kushirikisha jamii ikiwemo makundi maalum katika kuibua na kutekeleza vipaumbele vya kupunguza vihatarishi vya maafa; na

(iii) Wananchi kushiriki katika program za utunzaji wa mazingira ili kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi.

**Shabaha**

(i). Ujuzi wa jamii kwenye masuala ya usimamizi wa maafa kutambuliwa ifikapo, 2027;

(ii). Ujuzi wa jamii kutumika katika utekelezaji wa shughuli za upunguzaji vihatarishi vya maafa katika jamii ifikapo Juni, 2027;

(iii). Mpango wa utekelezaji wa vipaumbele vya upunguzaji wa vihatarishi vya maafa kwa kushirikisha jamii kuandaliwa na kutekelezwa ifikapo Juni, 2027;

(iv). Elimu kuhusu utunzaji wa mazingira kutolewa kwa jamii ifikapo Juni, 2027; na

(v). Jamii kuhamasishwa na kushiriki katika shughuli za utunzaji wa mazingira zitakazochangia kupunguza vihatarishi vya maafa ifikapo Juni, 2027.

**Jedwali 5: Bangokititia la Utekelezaji wa Mkakati**

| Lengo | Mikakati | Shabaha | Bajeti | Muda wa Utekelezaji | Mhusika |
|---|---|---|---|---|---|
| Kuongeza uelewa wa upunguzaji wa vihatarishi vya maafa kwa jamii, sekta na wadau katika ngazi ya wilaya; | Kujenga uelewa kuhusu masuala ya upunguzaji wa vihatarishi vya maafa kwa kamati za usimamizi wa maafa, wadau na jamii; | Elimu kwa Kamati za Usimamizi wa Maafa ngazi ya Wilaya hadi Kijiji kutolewa ifikapo 2027; | 53,500,000 | Miaka 5 | Halmashauri kwa kushirikiana na Wadau |
| | | Uhamasishaji wa kukuza uelewa wa vihatarishi vya maafa kwenye maeneo hatarishi kufanyika ifikapo Juni, 2027; | 7,500,000 | Miaka 5 | DED |
| | Kufanya tathmini za kabla, wakati na baada ya maafa kutokea katika Wilaya; | Maeneo hatarishi kubainishwa ifikapo, Juni 2027; | 10,000,000 | Mwaka 1 | DED |
| | | Uwezo wa Halmashauri Kukabili na kubaini Maafa ifikapo Juni, 2027; | 12,500,000 | Miaka 5 | DED |
| | | Tathmini za uharibifu na mahitaji wakati wa maafa kufanyika ifikapo Juni, 2027; | 20,000,000 | Miaka 5 | Halmashauri kwa kushirikiana na Wadau |

| Lengo | Mikakati | Shabaha | Bajeti | Muda wa Utekelezaji | Mhusika |
|---|---|---|---|---|---|
| | | Uharibifu na hasara kutokana na maafa kutambuliwa ifikapo juni, 2027; | 12,500,000 | Miaka 5 | DED |
| | Kufanya tafiti za Vihatarishi vya Maafa kwa kushirikiana na wadau mbalimbali wa usimamizi wa maafa waliopo katika Wilaya; | Tafiti za visababishi vya maafa yanayojirudia kufanyika ifikapo Juni, 2027; | 12,500,000 | Miaka 5 | DED |
| | Wilaya kukuza matumizi ya TEHAMA na huduma za kijiografia katika usimamizi wa vihatarishi vya maafa. | Mifumo ya TEHAMA kutumika katika usimamizi wa maafa ifikapo Juni, 2027; | 10,000,000 | Miaka 5 | DED |
| | | Ramani za maeneo hatarishi na maeneo ya uhamishaji kuandaliwa ifikapo Juni, 2027; | 22,500,000 | Miaka 5 | DED |
| Kuboresha mfumo wa tahadhari ya awali ili kujiandaa na majanga mbalimbali na utoaji wa taarifa zenye kujikita katika jamii. | Kutumia maarifa ya asili kwenye mfumo wa utoaji wa tahadhari ya awali; | Maarifa na mbinu za kiasili zinazotumika kupata tahadhari ya awali kubainishwa ifikapo Juni, 2027; | 10,000,000 | Miaka 5 | DED |
| | | Maarifa na mbinu za asili kuboreshwa na kujumuishwa kwenye mfumo rasmi wa utoaji wa tahadhari ifikapo | 8,000,000 | Miaka 5 | DED |

| Lengo | Mikakati | Shabaha | Bajeti | Muda wa Utekelezaji | Mhusika |
|---|---|---|---|---|---|
| | | Juni 2027; | | | |
| | Kuwepo na mfumo rasmi wa utoaji na upokeaji wa taarifa za tahadhari ya awali kuanzia ngazi ya Halmashauri, kata na kijiji, na jamii kwa ujumla; | Taratibu za uendeshaji na itifaki kwa ajili ya utoaji na usambazaji wa tahadhari za awali kuandaliwa ifikapo Juni, 2027; | 7,500,000 | Miaka 5 | DED |
| Kuimarisha uwezo wa kuzuia, kupunguza vihatarishi na kujiandaa kukabiliana na maafa ili kujenga ustahimilivu katika jamii. | Kuandaa na kutekeleza programu za upunguzaji wa vihatarishi vya majanga yanayoikumba Halmashauri; | Mpango wa matumizi bora ya ardhi kutekelezwa ifikapo Juni, 2027 | 10,000,000 | Miaka 5 | Wadau |
| | | Watu wanaoishi katika maeneo hatarishi kutambuliwa na kuhamishwa ifikapo Juni, 2027; | 8,000,000 | Miaka 5 | DED |
| | | Programu za mafunzo ya kupunguza vihatarishi ya majanga kutekelezwa ifikapo Juni, 2027; | 9,500,000 | Miaka 5 | DED |
| | Kutambua rasilimali zinazoweza | Kanzidata ya wadau na | 16,000,000 | Miaka 5 | DED |

| Lengo | Mikakati | Shabaha | Bajeti | Muda wa Utekelezaji | Mhusika |
|---|---|---|---|---|---|
| | kutumika kukabiliana na maafa katika Halmashauri; | rasilimali za kukabiliana na maafa kuandaliwa ifikapo Juni, 2027; | | | |
| | | Timu za utafutaji na uokoaji kuanzishwa ifikapo Juni, 2027; | 7,500,000 | Miaka 5 | DED |
| | Kufanya mazoezi ya vitendo ya kwa ajili ya kujiandaa na kukabili maafa; | Mazoezi ya mezani na vitendo ya kujiandaa na kukabili maafa kufanyika ifikapo Juni, 2027; | 15,000,000 | Miaka 5 | Halmashauri kwa kushirikiana na Wadau |
| | Kuimarisha huduma za utafutaji na uokoaji katika Halmashauri kwa kuzingatia majanga yaliyopo; | Njia za kupita wakati wa uhamishaji kuainishwa ifikapo Juni, 2027; | 7,500,000 | Miaka 5 | DED |
| | | Maeneo salama kwa ajili ya kuhamishia watu wakati wa dharura kutambuliwa na kutengwa ifikapo Juni, 2027; | 15,000,000 | Miaka 5 | DED |
| | | Maeneo yanayofaa kwa ajili ya huduma ya matibabu ya dharura kwa magonjwa ya | 5,000,000 | Miaka 5 | Halmashauri kwa kushirikian |

| Lengo | Mikakati | Shabaha | Bajeti | Muda wa Utekelezaji | Mhusika |
|---|---|---|---|---|---|
| | | mlipuko kutambuliwa na kutengwa ifikapo Juni, 2027; | | | a na Wadau |
| Kuimarisha uwezo wa kukabili na kurejesha hali baada ya maafa kutokea. | Kufanya tathmini za uharibifu na mahitaji baada ya maafa kutokea; | Tathmini ya haraka ya uharibifu na mahitaji wakati wa maafa kufanyika ifikapo Juni, 2027; | 7,500,000 | Miaka 5 | DED |
| | | Tathmini ya kina ya uharibifu na mahitaji baada ya maafa kufanyika ifikapo Juni, 2027; | 7,500,000 | Miaka 5 | DED |
| | Kuhamasisha upatikanaji wa rasilimali kwa ajili ya kukabiliana na kurejesha hali baada ya maafa; | Wadau kuhamasishwa kushiriki na kutoa rasilimali kwa ajili ya operesheni za kukabiliana na maafa ifikapo Juni, 2027; | 7,500,000 | Miaka 5 | Halmashauri kwa kushirikiana na Wadau |
| | Kutekeleza muongozo wa utoaji wa huduma za kibinadamu wakati wa maafa; | Huduma za kibinadamu kwa waathirika wa maafa kutolewa kwa kuzingatia muongozo ifikapo Juni, 2027; | 12,500,000 | Miaka 5 | DED |

| Lengo | Mikakati | Shabaha | Bajeti | Muda wa Utekelezaji | Mhusika |
|---|---|---|---|---|---|
| | | Huduma za usaidizi wa kisaikolojia na kurekebisha afya ya akili kwa waathirika wa maafa na watoa huduma kutolewa ifikapo Juni, 2027; | 7,500,000 | Miaka 5 | DED |
| Kujenga ustahimilivu kwa jamii kupitia ushirikishaji na uwajibikaji wa wanajamii katika kuzuia, kupunguza, kujiandaa na kukabili maafa; | Kutumia ujuzi wa jamii katika kuzuia, kupunguza, kujiandaa, kukabili maafa na kurejesha hali baada ya maafa; | Ujuzi wa jamii kwenye masuala ya usimamizi wa maafa kutambuliwa ifikapo, 2027; | 5,000,000 | Miaka 5 | DED |
| | | Ujuzi wa jamii kutumika katika utekelezaji wa shughuli za upunguzaji vihatarishi vya maafa katika jamii ifikapo Juni, 2027; | 5,000,000 | Miaka 5 | DED |
| | Kushirikisha jamii ikiwemo makundi maalum katika kuibua vipaumbele vya kutekelezwa ili kupunguza vihatarishi vya maafa; | Mpango wa utekelezaji wa vipaumbele vya upunguzaji wa vihatarishi vya maafa kwa kushirikisha jamii kuandaliwa na kutekelezwa ifikapo Juni, 2027; | 7,500,000 | Miaka 5 | DED |

| Lengo | Mikakati | Shabaha | Bajeti | Muda wa Utekelezaji | Mhusika |
|---|---|---|---|---|---|
| | Wananchi kushiriki katika program za utunzaji wa mazingira ili kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi; | Elimu kuhusu utunzaji wa mazingira kutolewa kwa jamii ifikapo Juni, 2027; na | 7,500,000 | Miaka 5 | Halmashauri kwa kushikiana na Wadau |
| | | Jamii kuhamasishwa na kushiriki katika shughuli za utunzaji wa mazingira zitakazochangia kupunguza vihatarishi vya maafa ifikapo Juni, 2027 | 7,500,000 | Miaka 5 | Halmashauri kwa kushirikiana na Wadau |
| | JUMLA | | 354,500,000/= | | |

## SEHEMU YA TANO:

### 5.1 Mfumo wa Ufuatiliaji na Tathmini

Mfumo wa Ufuatiliaji na Tathmini umeundwa ili kufuatilia maendeleo na kutathmini utekelezaji wa Mkakati wa Upunguzaji wa Vihatarishi vya Maafa katika Halmashauri ya Wilaya ya Rufiji. Jukumu la jumla la ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa Mkakati ni la Halmashauri ya Wilaya ya Rufiji kwa ushirikiano wa karibu na wadau wengine.

Kila mdau anayehusika na utekeleazaji wa Mkakati atakuwa na wajibu wa kutoa taarifa ya utekelezaji wa malengo na shabaha kwa Halmashauri ya Wilaya. Msisitizo ni kuhakikisha malengo na shabaha zinafikiwa kwa kuzingatia muda na bajeti ya shughuli zilizoainishwa kwa utekelezaji. Aidha ufuatiliaji utafanywa kupitia mikutano, taarifa mahususi za jumla, usimamizi na ukaguzi.

**Lengo Kuu la mfumo wa ufuatiliaji na tathmini**

Kufuatilia na kupima utekelezaji wa malengo ya Mkakati wa Kupunguza Vihatarishi vya Maafa ili kuhakikisha kuwa yanafikiwa ipasavyo.

**Malengo mahsusi.**

- Kufuatilia utekelezaji wa mkakati wa kupunguza hatari ya maafa katika Halmashauri kulingana na malengo na shabaha zilizoainishwa;
- Kuweka vigezo vya upatikanaji wa taarifa na takwimu za utekelezaji ili kupunguza vihatarishi vya maafa katika Halmashauri;
- Kubaini endapo matokeo ya mkakati yanasaidia kupunguza vihatarishi vya maafa;
- Kubaini endapo rasilimalizi zilizopo zinatumika kwa ufanisi ili kufikia malengo;
- Kubaini changamoto zilizopo katika utekelezaji wa mkakati kwenye Halmashauri; na
- Kuweka mfumo wa kupokea na kupashana taarifa katika ngazi zote.

### 5.2 Viashiria vya Utendaji na Matokeo Tarajiwa

**Jedwali 6: Viashiria vya utendaji wa mfumo wa ufuatiliaji na tathmini**

| **Malengo** | **Viashiria vya Matokeo** | **Matokeo** |
|---|---|---|
| Kuongeza uelewa wa | - Idadi ya Kamati za Usimamizi wa Maafa | -Ongezeko la uelewa kwenye masuala ya |

| | | |
|---|---|---|
| upunguzaji wa vihatarishi vya maafa kwa jamii, sekta na wadau katika ngazi ya wilaya; | ngazi ya kata na kijiji zilizopatiwa Elimu;<br>- Idadi ya matukio ya uhamasishaji yaliyofanyika kwenye maeneo hatarishi;<br>- Idadi ya maeneo hatarishi yaliyobainishwa;<br>- Idadi ya Tathmini za uharibifu na mahitaji wakati wa maafa zilizofanyika;<br>- Idadi ya tathmini zauharibifu na hasara baada ya maafa zilizofanyika;<br>- Idadi ya tafiti za visababishi vya maafa yanayojirudia zilizofanyika;<br>- Mifumo ya TEHAMA inayotumika katika kutekeleza shughuli za usimamizi wa maafa; na<br>- Ramani za maeneo hatarishi na maeneo zilizoandaliwa; | usimamizi wa maafa<br>-Jamii itazingatia upunguzaji wa vihatarishi vya maafa kwenye shughuli zao za kila siku<br>-Kupungua kwa kiwango cha uharibifu na hasara kutokana na maafa<br>-Upatikanaji wa taarifa za usimamizi wa maafa kwa wakati<br>-Mipango ya maendeleo kutekelezwa kwa kuzingatia vihatarishi vilivyopo |
| Kuboresha mfumo wa tahadhari ya awali ili kujiandaa na majanga mbalimbali na utoaji wa taarifa zenye kujikita katika jamii. | - Idadi ya mbinu za kiasili zinazotumika katika mfumo rasmi wa tahadhari;<br>- Taratibu za uendeshaji na itifaki kwa ajili ya utoaji na usambazaji wa tahadhari zilizoandaliwa; | -Kupungua kwa madhara ya maafa kwa jamii |
| Kuimarisha uwezo wa kuzuia, kupunguza | - Shughuli zinazotekelezwa kwa kuzingatia Mpango wa matumizi bora ya ardhi; | -Kuimarika kwa ustahimilivu wa jamii dhidi ya maafa.<br>-Kupungua kwa matukio |

| | | |
|---|---|---|
| vihatarishi na kujiandaa kukabiliana na maafa ili kujenga ustahimilivu katika jamii. | - Idadi ya watu wanaoishi kwenye maeneo hatarishi waliotambuliwa;<br>- Idadi ya watu wanaoishi kwenye maeneo hatarishi waliohamishwa;<br>- Programu za mafunzo ya kupunguza vihatarishi ya majanga zilizotekelezwa;<br>- Kanzidata ya wadau na rasilimali za kukabiliana na maafa iliyoandaliwa;<br>- Timu za utafutaji na uokoaji zilizoundwa;<br>- Idadi ya mazoezi ya mezani na vitendo ya kujiandaa na kukabili maafa yaliyofanyika;<br>- Njia za kupita wakati wa uhamishaji zilizoainishwa;<br>- Idadi ya maeneo salama kwa ajili ya kuhamishia watu wakati wa dharura yaliyotambuliwa na kutengwa; na<br>- Idadi ya maeneo yanayofaa kwa ajili ya huduma ya matibabu ya dharura kwa magonjwa ya mlipuko yaliyotambuliwa na kutengwa. | ya maafa<br>-Ongezeko la ushiriki wa wadau katika kukabili maafa |
| Kuimarisha uwezo wa kukabili na kurejesha hali baada ya maafa kutokea | - Idadi ya tathmini za haraka za uharibifu na mahitaji wakati wa maafa zilizofanyika<br>- Idadi ya tathmini za kina za uharibifu na hasara baada ya maafa zilizofanyika<br>- Idadi ya wadau walioshiriki operesheni za | -Kupungua madhara ya maafa<br>-Kuimarika kwa ustahimilivu wa jamii kwa kurejesha kwa ubora zaidi |

| | | |
|---|---|---|
| | kukabili maafa<br>- Rasilimali zilizochangiwa na wadau<br>- Idadi ya matukio ya uhamasishaji yaliyofanyika<br>- Huduma za kibinadamu kwa waathirika wa maafa zilizotolewa;<br>- Idadi ya vipindi vya huduma za usaidizi wa kisaikolojia na kurekebisha afya ya akili kwa waathirika wa maafa vilivyotolewa | |
| Kujenga ustahimilivu kwa jamii kupitia ushirikishaji na uwajibikaji wa wanajamii katika kuzuia, kupunguza, kujiandaa na kukabili maafa; | - Ujuzi wa jamii kwenye masuala ya usimamizi wa maafa uliotambuliwa<br>- Ujuzi wa jamii uliotumika katika utekelezaji wa shughuli za upunguzaji vihatarishi vya maafa<br>- Mpango wa utekelezaji wa vipaumbele vya upunguzaji wa vihatarishi vya maafa kwa kushirikisha jamii ulioandaliwa<br>- Elimu kuhusu utunzaji wa mazingira iliyotolewa<br>- Idadi ya matukio ya uhamasishaji yaliyofanyika<br>- Shughuli za utunzaji wa mazingira ambazo jamii inashiriki | -Ongezeko la ushiriki wa jamii kwenye matukio ya upunguzaji wa vihatarishi vya maafa<br>-Uwepo wa mazingira bora kwa maendeleo endelevu |

## 5.3 Mpango wa Ufuatiliaji

Ufuatiliaji wa utekelezaji wa mkakati huu utafanyika kila robo mwaka. Ufuatiliaji utafanyika kama sehemu ya kawaida ya utekelezaji wa shughuli za Serikali ambao hufanyika kila robo mwaka.

Mpango wa ufuatiliaji kwa mwaka utafanyika kwa kuzingatia mpango ulioanishwa katika Jedwali Na.7 hapa chini.

## Jedwali 7: Mpango wa Ufuatiliaji

| SN | KIASHIRIA | TAKWIMU ZILIZOPO (BASELINE) | | KIASI/IDADI YA KIASHIRIA KATIKA KUFIKIA SHABAHA | | | | | NJIA YA UKUSANYAJI TAARIFA/TAKWIMU | | MHUSIKA WA KUKUSANYA TAARIFA/TAKWIMU |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | MWAKA | KIASI/ IDADI | M1 | M2 | M3 | M4 | M5 | CHANZO CHA TAARIFA | MBINU/ZANA ZA KUKUSANYIA DATA/TAARIFA | |
| 1. | Idadi ya Kamati za Usimamizi wa Maafa ngazi ya Wilaya hadi Kijiji zilizopatiwa Elimu; | 2022/27 | 53 | 9 | 10 | 10 | 12 | 12 | Idara ya mipango | Vikao kazi vya Kamati za maafa | Kamati ya wataalamu kwa kushirikiana na Wadau |
| 2. | Idadi ya matukio ya uhamasishaji yaliyofanyika kwenye maeneo hatarishi; | 2022/27 | 20 | 4 | 4 | 4 | 4 | 4 | Ofisi za Kata na Vijiji | Mkutano wa Vijiji | Kamati za maafa kata na vijiji |
| 3. | Idadi ya maeneo hatarishi yaliyobainishwa; | 2022/27 | 20 | 4 | 4 | 4 | 4 | 4 | Idara ya Mipango | Makundi maalumu | Kamati ya wataalamu kwa kushirikiana na Kamati ya kata na vijiji. |
| 4. | Idadi Tathmini za uharibifu na mahitaji wakati wa maafa zilizofanyika; | 2022/27 | 10 | 2 | 2 | 2 | 2 | 2 | Idara ya Mipango | Makundi maalumu | Kamati ya wataalamu kwa kushirikiana na Kamati ya kata na vijiji. |
| 5. | Idadi ya tathmini za uharibifu na hasara baada ya maafa zilizofanyika; | 2022/27 | 10 | 2 | 2 | 2 | 2 | 2 | Idara ya Mipango | Makundi Maalumu | Kamati ya wataalamu kwa kushirikiana na Kamati |

| SN | KIASHIRIA | TAKWIMU ZILIZOPO (BASELINE) | | KIASI/IDADI YA KIASHIRIA KATIKA KUFIKIA SHABAHA | | | | | NJIA YA UKUSANYAJI TAARIFA/TAKWIMU | | MHUSIKA WA KUKUSANYA TAARIFA/TAKWIMU |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | MWAKA | KIASI/ IDADI | M1 | M2 | M3 | M4 | M5 | CHANZO CHA TAARIFA | MBINU/ZANA ZA KUKUSANYIA DATA/TAARIFA | |
| | | | | | | | | | | | ya kata na vijiji. |
| 6. | Idadi ya tafiti za visababishi vya maafa yanayojirudia zilizofanyika; | 2022/27 | 5 | 1 | 1 | 1 | 1 | 1 | Idara ya Mipango | Kutumia Madodoso | Kamati ya Wataalamu kwa kushirikiana na Wadau |
| 7. | Mifumo ya TEHAMA inayotumika katika kutekeleza shughuli za usimamizi wa maafa. | 2022/27 | 10 | 2 | 2 | 2 | 2 | 2 | Kitengo cha TEHAMA | GPS | Kitengo cha TEHEMA |
| 8. | Ramani za maeneo hatarishi na maeneo zilizoandaliwa; | 2022/27 | 38 | 3 | 8 | 9 | 9 | 9 | Idara ya Ardhi | Mikutano ya Kata na Vijiji | Idara ya Ardhi |
| 9. | Idadi ya mbinu za kiasili zinazotumika katika mfumo rasmi wa tahadhari; | 2022/27 | 15 | 3 | 3 | 3 | 3 | 3 | Ofisi ya Kata na Kijiji | Kutumia makundi mbalimbali ya jamii | Kamati ya Maafa ya kata na vijiji |
| 10. | Taratibu za uendeshaji na itifaki kwa ajili ya utoaji na usambazaji wa tahadhari za zilizoandaliwa; | 2022/27 | 1 | | 1 | 6 | 3 | 4 | Ofisi ya Kata na Kijiji | Kutumia makundi mbalimbali ya jamii | Kamati ya Maafa ya kata na vijiji |
| 11. | Shughuli zinazotekelezwa kwa kuzingatia Mpango wa matumizi bora ya ardhi; | 2022/27 | 10 | 2 | 2 | 2 | 2 | 2 | Idara ya Ardhi | Mikutano ya Kata na Vijiji | Idara ya Ardhi |
| 12. | Idadi ya watu wanaoishi kwenye maeneo hatarishi waliotambuliwa; | 2022/27 | 2 | 1 | | 1 | 2 | 4 | Ofisi ya kata na vijiji | Mikutano ya kata na vijiji | Kamati za Maafa kata na vijiji |
| 13. | Idadi ya watu wanaoishi kwenye maeneo hatarishi waliohamishwa; | 2022/27 | 10 | 2 | 2 | 2 | 2 | 2 | Idara ya Mipango | Mikutano ya kata na Vijiji | Kamati ya Wataalam ,Ofisi ya Kata na vijiji. |

| SN | KIASHIRIA | TAKWIMU ZILIZOPO (BASELINE) | | KIASI/IDADI YA KIASHIRIA KATIKA KUFIKIA SHABAHA | | | | | NJIA YA UKUSANYAJI TAARIFA/TAKWIMU | | MHUSIKA WA KUKUSANYA TAARIFA/TAKWIMU |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | MWAKA | KIASI/ IDADI | M1 | M2 | M3 | M4 | M5 | CHANZO CHA TAARIFA | MBINU/ZANA ZA KUKUSANYIA DATA/TAARIFA | |
| 14. | Programu za mafunzo ya kupunguza vihatarishi ya majanga zilizotekelezwa; | 2022/27 | 20 | 4 | 4 | 4 | 4 | 4 | Idara ya Mipango | Kutumia Vikao kazi | Kamati ya Wataalam kwa kushirikiana na Wadau. |
| 15. | Kanzidata ya wadau na rasilimali za kukabiliana na maafa iliyoandaliwa; | 2022/27 | 2 | 1 | | 1 | | | Idara ya Mipango | Kutumia Madodoso | Kamati ya Wataalam kwa kushirikiana na Wadau. |
| 16. | Timu za utafutaji na uokoaji zilizoundwa; | 2022/27 | 1 | 1 | | | | | Idara ya Mipango | Kutumia makundi maalum | Kamati ya Wataalam |
| 17. | Idadi ya mazoezi ya mezani na vitendo ya kujiandaa na kukabili maafa yaliyofanyika; | 2022/27 | 10 | 1 | 2 | 2 | 2 | 3 | Idara ya Mipango | Mahojiano | Jeshi la zima moto na uokoaji. |
| 18. | Njia za kupita wakati wa uhamishaji zilizoainishwa; | 2022/27 | 1 | | 1 | | | | Ofisi za kata na vijiji | Kutumia Mikutano | Kamati za kata na vijiji |
| 19. | Idadi ya maeneo salama kwa ajili ya kuhamishia watu wakati wa dharura yaliyotambuliwa na kutengwa; na | 2022/27 | 38 | 38 | | | | | Idara ya Mipango | Kutumia Mikutano | Idara ya Ardhi |
| 20. | Idadi ya maeneo yanayofaa kwa ajili ya huduma ya matibabu ya dharura kwa magonjwa ya mlipuko yaliyotambuliwa na kutengwa. | 2022/27 | 38 | 38 | | | | | Idara ya Afya | Kutumia Mikutano | Kamati za kata na vijiji |
| 21. | Idadi ya tathmini za haraka za uharibifu na mahitaji wakati wa maafa zilizofanyika | 2022/27 | 10 | 2 | 2 | 2 | 2 | 2 | Idara ya Mipango | Mahojiano | Kamati za kata na vijiji . |
| 22. | Idadi ya tathmini za kina za uharibifu na hasara baada ya maafa zilizofanyika | 2022/27 | 10 | 2 | 2 | 2 | 2 | 2 | Idara ya Mipango | Mahojiano | Kamati za kata na vijiji na wataalam |

| SN | KIASHIRIA | TAKWIMU ZILIZOPO (BASELINE) | | KIASI/IDADI YA KIASHIRIA KATIKA KUFIKIA SHABAHA | | | | | NJIA YA UKUSANYAJI TAARIFA/TAKWIMU | | MHUSIKA WA KUKUSANYA TAARIFA/TAKWIMU |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | MWAKA | KIASI/ IDADI | M1 | M2 | M3 | M4 | M5 | CHANZO CHA TAARIFA | MBINU/ZANA ZA KUKUSANYIA DATA/TAARIFA | |
| 23. | Idadi ya wadau walioshiriki operesheni za kukabili maafa | 2022/27 | 5 | 1 | 1 | 1 | 1 | 1 | Idara ya Mipango | Vikao kazi | Kamati ya wataalamu na Wadau |
| 24. | Rasilimali zilizochangiwa na wadau | 2022/27 | 5 | 1 | 1 | 1 | 1 | 1 | Idara ya Mipango | Mahojiano | Kamati elekezi na Wadau |
| 25. | Idadi ya matukio ya uhamasishaji yaliyofanyika | 2022/27 | 20 | 4 | 4 | 4 | 4 | 4 | Idara ya Mipango | Mikutano ya Kata na vijiji | Kamati elekezi na Wadau |
| 26. | Huduma za kibinadamu kwa waathirika wa maafa zilizotolewa; | 2022/27 | 10 | 2 | 2 | 2 | 2 | 2 | Idara Mipango na Afya | Jamii na vitabu vya MTUHA | Kamati ya Wataalam na Wadau |
| 27. | Idadi ya vipindi vya huduma za usaidizi wa kisaikolojia na kurekebisha afya ya akili kwa waathirika wa maafa vilivyotolewa | 2022/27 | 10 | 2 | 2 | 2 | 2 | 2 | Idara Mipango na Afya | Jamii na vitabu vya MTUHA | Kamati ya Wataalam na Wadau |
| 28. | Ujuzi wa jamii kwenye masuala ya usimamizi wa maafa uliotambuliwa | 2022/27 | 5 | 1 | 1 | 1 | 1 | 1 | Ofisi ya Kata na vijiji | Mikutano ya hadhara | Kamati za kata na vijiji |
| 29. | Ujuzi wa jamii uliotumika katika utekelezaji wa shughuli za upunguzaji vihatarishi vya maafa | 2022/27 | 5 | 1 | 1 | 1 | 1 | 1 | Ofisi ya Kata na vijiji | Mikutano ya hadhara | Kamati za kata na vijiji |
| 30. | Mpango wa utekelezaji wa vipaumbele vya upunguzaji wa vihatarishi vya maafa kwa kushirikisha jamii ulioandaliwa | 2022/27 | 5 | 1 | 1 | 1 | 1 | 1 | Idara ya Mipango | Kutumia Mikutano ya vijiji na kata | Kamati za Wataalam, Kata na vijiji |
| 31. | Elimu kuhusu utunzaji wa mazingira iliyotolewa | 2022/27 | 10 | 2 | 2 | 2 | 2 | 2 | Idara ya Mipango | Kutumia Mikutano ya vijiji na kata | Kamati za Wataalam, Kata na vijiji |
| 32. | Idadi ya matukio ya uhamasishaji yaliyofanyika | 2022/27 | 10 | 2 | 2 | 2 | 2 | 2 | Idara ya Mipango | Kutumia Mikutano ya vijiji na kata | Kamati elekezi na Wadau |

| SN | KIASHIRIA | TAKWIMU ZILIZOPO (BASELINE) | | KIASI/IDADI YA KIASHIRIA KATIKA KUFIKIA SHABAHA | | | | | NJIA YA UKUSANYAJI TAARIFA/TAKWIMU | | MHUSIKA WA KUKUSANYA TAARIFA/TAKWIMU |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | MWAKA | KIASI/ IDADI | M1 | M2 | M3 | M4 | M5 | CHANZO CHA TAARIFA | MBINU/ZANA ZA KUKUSANYIA DATA/TAARIFA | |
| 33. | Shughuli za utunzaji wa mazingira ambazo jamii inashiriki | 2022/27 | 10 | 2 | 2 | 2 | 2 | 2 | Idara ya Mipango | Kutumia Mikutano hadhara | Kitengo cha Mazingira |

## 5.4 Utoaji wa Taarifa

Eneo hili linahusu utoaji wa taarifa ndani na nje ya Halmashauri ya Wilaya ya Rufiji. Mpango wa utoaji taarifa umeandaliwa kwa kuzingatia mfumo wa utoaji taarifa ulioanishwa kwenye Sheria ya Usimamizi wa Maafa Sura ya 242, Miongozo ya Mipango na Bajeti na utaratibu mwingine wa uandaaji na utoaji taarifa uliopo katika Wilaya.

Halmashauri itaunganisha taarifa za utekelezaji wa shughuli mbalimbali kutoka katika ngazi ya kata na kijiji na kutoka kwa wadau na taasisi zilizopo katika halmashauri ili kutoa taarifa za utendaji za robo mwaka, nusu mwaka na mwaka. Taarifa hizi zitashirikishwa kwa wadau wa Upunguzaji wa Vihatarishi vya Maafa kwa ajili ya mapitio, majadiliano na kupanga upya utekelezaji.

### 5.4.1 Mpango wa Ndani wa Utoaji Taarifa

Mpango wa ndani wa utoaji taarifa unaundwa na ngazi tatu za utoaji taarifa, ikijumuisha taarifa za idara/vitengo vya Halmashauri, taarifa za taasisi na wadau walio kwenye Halmashauri, na Taarifa za Menejimenti kwa ajili ya kuwasilishwa kwenye Kamati ya Usimamizi wa Maafa. Taarifa zitaandaliwa kwa robo mwaka, nusu mwaka na taarifa za mwaka na kuwasilishwa kwa wadau wa ndani.  Mpango umeanishwa kwenye Jedwali Na.8 hapa chini.

**Jedwali 8: Mpango wa Ndani wa Utoaji Taarifa**

| NA. | Chanzo cha Taarifa | Aina ya Taarifa | Mpokeaji | Muda | Mhusika |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Idara | Taarifa za utekelezaji wa Mkakati wa Upunguzaji Vihatarishi vya Maafa katika ngazi ya idara | Mkuu wa Idara | Robo Mwaka | Wakuu wa Idara |
| 2 | Wakuu wa Idara | Taarifa za utekelezaji wa Mkakati wa Upunguzaji Vihatarishi vya Maafa katika ngazi ya idara | Mkuu wa Idara ya Mipango | Robo Mwaka, Nusu Mwaka | Mkuu wa Idara ya Mipango |
| 3 | Kamati ya Wataalam wa Usimamizi wa Maafa | Taarifa ya utekelezaji wa Mkakati | Kamati Elekezi ya Usimaizi wa Maafa ya Wilaya | Robo mwaka, Nusu mwaka, Mwaka. | Mkurugenzi wa Halmashauri |

### 5.4.2 Mpango wa Utoaji Taarifa Nje ya Halmashauri (Mkoa na Taifa)

Mpango wa utoaji taarifa unajumuisha utoaji wa taarifa za robo mwaka, nusu mwaka na taarifa za mwaka na kuwasilishwa Ofisi ya Mkuu wa Mkoa na Ofisi ya Waziri Mkuu. Mpango umeanishwa kwenye Jedwali Na.9 hapa chini.

**Jedwali 9: Mpango wa Utoaji Taarifa Nje ya Halmashauri**

| NA. | Chanzo cha Taarifa | Aina ya Taarifa | Mpokeaji | Muda | Mhusika |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Kamati Elekezi ya Usimaizi wa Maafa ya Wilaya | Taarifa za utekelezaji wa Mkakati wa Upunguzaji Vihatarishi vya Maafa katika ngazi ya idara | Ofisi ya Mkuu wa Mkoa | Robo mwaka, Nusu mwaka, Mwaka. | Mkurugenzi wa Halmashauri |
| 2 | Ofisi ya Mkuu wa Mkoa | Taarifa za utekelezaji wa Mkakati wa Upunguzaji Vihatarishi vya Maafa katika ngazi ya idara | Ofisi ya Waziri Mkuu | Robo mwaka, Nusu mwaka, Mwaka. | Katibu Tawala Mkoa |

## SEHEMU YA SITA

### 6.1 Mfumo wa Usimamizi wa Maafa

Mkakati huu umeandaliwa kwa kuzingatia Sera, Sheria, Mifumo, Makubaliano, miongozo ya kitaifa inayohusu upunguzaji na usimamizi wa vihatarishi vya maafa.

### 6.2 Sera ya Taifa ya Menejimenti ya Maafa 2004


Sera inatamka kuanzishwa kwa Kamati za Wilaya za Usimamizi wa Maafa ambazo zinawajibika katika kuzuia na kupunguza vihatarishi vya majanga pamoja na kujiandaa, kukabiliana na kurejesha hali pindi maafa yanapotokea. Aidha, sera inatoa wito wa ushirikiano wa kisekta katika shughuli za usimamizi wa vihatarishi vya maafa na utoaji wa huduma za kibinadamu kwa kuwa suala hili ni mtambuka.

### 6.3 Sheria ya Usimamizi wa Maafa Sura 242

Sheria inaelekeza kuanzishwa kwa Kamati za Usimamizi wa Maafa katika ngazi ya Wilaya, Kata na Kijiji. Kamati zina jukumu la kusimamia masuala yote ya usimamizi wa maafa katika ngazi husika.

### 6.4 Muundo wa Usimamizi wa Maafa Katika Halmashauri

Muundo wa usimamizi wa maafa katika Halmashauri ya Wilaya umeainishwa katika mchoro Na.1 hapa chini.




**Mchoro 1: Muundo wa Usimamizi wa Maafa Tanzania**